Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

kini nasema, Hawakusikia ? Yakini, Hatta
inchi yote imetoka sauti yao, na hatta mi-
19 paka ya ulimwengu maneno yao. Lakini
nasema, Israeli hakujua ? Kwanza Musa
anasema, Nitawatia uwivu kwao wasio taifa
na kwa taifa wasio na akili nitawakasirisha.
20 Isaya hakuogopa, akasema, Nimeonwa nao
wasionitafuta mimi, nimeonekana nao wasi-
21 oniulizia. Kwa Israeli anasema, Mchana
kutwa nimewanyoshea mikono watu wasio-
amini na wasiokubali.

XI. Nasema tena, Muungu amewatupa watu
wake ? Hasha. Kwani na mimi ni Mwi-
sraeli, katika wazao wa Ibrahimu, kabila
2 ya Benyamin. Hakutupa Muungu watu
wake aliotangulia kuwajua. Hamjui ya
Eliya yasemaje maandiko, kama alivyowa-
3 nenea Israeli kwa Muungu, Bwana, nabii
zako wamewaua, mathbahu zako wameyaa-
ngusha, nami nimesalia peke yangu, nao
4 wanatafuta roho yangu. Lakini aambiwaje
na jawabu ? Nimejiwekea waume elfu sa-
5 ba, wasiokunja gote kwa Baal. Hivi na wa-
kati huu yamekuwa masalia kwa kuchagua



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

6 kwa neema. Ikiwa kwa neema, si tena kwa
matendo, neema isiishe kuwa neema; kama
kwa matendo, si tena kwa neema, matendo
yasiishe kuwa matendo.
7 Nini tena? Waitafutayo Israeli, hawa-
kuiona, waliochaguliwa wameiona, waliosa-
8 lia wakatiwa ugumu, kama ilivyoandikwa,
Wakapewa na Muungu roho ya usingizi,
macho yasiyoona na masikio yasiyosikia,
9 hatta leo. Naye Daud anasema, Meza yao
iwe shabuka, na mtego, na jiwe la kujikwaa,
10 na thawabu kwao, macho yao yatiwe giza
wasione, ukawainamishe mgongo siku zote.
11 Nasema, Wamejikwaa illi waanguke?
Hasha. Lakini kwa anguko lao wokovu
12 wa mataifa, watiwe uwivu. Kosa lao likiwa
fayida ya ulimwengu, na upungufu wao fayi-
da ya mataifa, si zayidi sana utimilifu wao.
13 Kwani nasema nanyi wa mataifa, nikiwa
mimi mtume wa mataifa natukuza kazi ya-
14 ngu, nipate labuda kuwatia uwivu walio
15 mwili wangu, niwaokoe baathi yao. Kwa-
ni kuwatupa wao kukiwa kupatanisha uli-
mwengu, nini kuwakubali, illa uzima katika



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

16 wafu? Limbuko likiwa takatifu nacho chu-
ngu, shina likiwa takatifu nayo matawi.
17 Tawi zikikatika wewe mzetuni wa mwi-
tuni utiliwe mahali pao, ukashariki shina na
18 unono wa mzetuni, usijisifu juu ya tawi, u-
kijisifu, si wewe ulichukuaye shina, illa shi-
na wewe.
19 Bassi utasema, Tawi zimekatika nitiliwe
20 mimi. Vema, kwa kukosa kuamini zika-
katika, nawe wasimama kwa imani, usione
21 makuu, illa wogope. Kwani Muungu asi-
poziachia tawi zilizo kwa asili, asikuachie
wewe.
22 Angalia wema na uzito wa Muungu, kwao
walioanguka uzito, kwako wema, ukikaa
23 katika wema, illa na wewe utakatika. Na
hawa wasipokaa katika kutoa kuamini, wa-
tatiliwa, kwani Muungu aweza tena kuwa-
tilia hawa.
24 Kama wewe uliyekatika katika mzetuni
wa asili wa mwituni, juu ya asili ukatiliwa
katika mzetuni mwema, si zayidi hawa wa-
lio wa asili watiliwe katika mzetuni wao
wenyewe?



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

25 Kwani sipendi, ndugu, msijue siri hiyo,
msijione ndinyi wa akili, kama ugumu kwa
sehemu umewawia Israeli, hatta utimilifu wa
26 mataifa utakapoingia, na hivi Israeli wote
wataokoka, kama ilivyoandikwa, Atatoka
katika Sayuni aokoaye, atawageukia Yako-
27 bo unajisi, na hilo agano langu kwao, nita-
28 kapoondoa thambi zao. Katika anjili adui
kwa ajili yenu, katika kuchaguliwa wamepe-
29 ndwa kwa ajili za baba. Kwani makarimu
na mwito wa Muungu hauna kugeuka.
30 Kama ninyi kwanza hamkumwamini Mu-
ungu, mkapata rehema kwa kutoa kuamini
31 kwao, hivi na hawa sasa hawakuamini re-
hema yenu, illi na hawa wapate rehema.
32 Kwani Muungu amewafunga wote katika
kutoa kuamini awape wote rehema.
33 Ee vilindi vya utajiri na hekima, na ku-
jua kwa Muungu, hukumu zake hazitafu-
34 tikani na njia zake haziandikani. Nani
aliyemjua nia yake Bwana, ao nani aliye
35 mshauri wake ? Ao nani aliyemtolea, naye
36 atarudishiwa ? Kwani Yeye asili, na Yeye
njia, na Yeye mwisho wa yote. Utukufu



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

uwe kwake milele. Amin.
XII. Nawasihi ndugu, kwa huruma za Muu-
ngu, mtoe miili yenu thabihu iliyo hayi,
takatifu, kumpendeza Muungu, ibada yenu
2 ya akili, wala msifananishwe na dunia hii,
illa mgeuke kwa kufanya mpya nia zenu,
mpate kuthubutisha nini alipendalo Muu-
ngu lililo jema, na kupendeza, na kamilifu.
3 Namwambia killa mtu wa kwenu, kwa
neema niliyopewa, asijithanie kuliko iliyo-
mpasa kuthani, illa afikiri kwa kadiri kama
killa mtu aliyogawaniwa na Muungu cheo
4 cha imani. Kwani kama katika mwili
mmoja kuna viungo vingi wala viungo vyo-
5 te havinayo kazi moja; hivi sisi wengi tu-
mekuwa mwili mmoja katika Masiya, na
mmoja mmoja viungo sisi kwa sisi.
6 Tukiwa na makarimu kwa neema tuliope-
wa yasiyo mamoja, kama unabii, kwa kadiri
7 yake imani, kama ungoje, katika kungojea,
8 kama mkufunzi, katika kufundisha, kama
aonyaye, katika kuonya, atoaye, pasipo hila,
atawalaye, kwa bidii, arehemuye, katika
kufurahiwa.



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

9 Kupenda pasipo unafiki, mkilichukia
10 ovu, mkiambatana nalo jema. Katika kupe-
ndana shauko mtu kwa mtu. Katika he-
11 shima mkitanguliza wenzenu. Katika ma-
kusudi si wavivu, wepesi rohoni, wakimtu-
12 mikia Bwana. Katika kutaraja mkifurahi,
katika shidda mkivumilia, katika kuomba
13 mkitia moyo, mkigawanya kwa mahitaji
yao watakatifu, mkifuata kuwakaribisha
wageni.
14 'Mwabariki wawafukuzao, barikini, msi-
15 laani. Kufurahi nao wafurahio, kulia nao
16 waliao. Mkithania sawa ninyi kwa ninyi,
msiyathanie yaliyo juu, illa mfuatane nao
walio chini, msiwe na akili kwenu wenyewe,
17 msipomlipia mtu ovu kwa ovu, mkiandika
18 vema machoni pa watu wote, kama yamki-
ni, miongoni mwenu, mpatane na watu wo-
19 te, msipojilipiza haki, enyi niwapendao,
mkaiachia nafasi hasira, kwani imeandikwa,
Kisasi ni changu, mimi nitalipa, amenena
20 Bwana. Naye adui wako akiona njaa, mli-
she, akiona kiu mnyweshe, kwani ukifanya
hivi utamletea makaa ya moto mengi ki-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is